# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Tel: 255- (022) 2122722/3/4
Dar es Salaam,-TANZANIA

Nukushi:+225 (022)2130852
Barua pepe: dg@nbs.go.tz


*Unapojibu tafadhali taja*:
Kumb Na: NBS/S.40/21/457

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe:17 Oktoba, 2011

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI SEPTEMBA, 2011

### Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye namna ya ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kutengeneza Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index formula" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZEKA HADI ASILIMIA 16.8

### Jedwali 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa mwezi Septemba 2011 (Septemba 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Sept-2010 | Ago - 2011 | Sept - 2011 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 100.00 | 118.50 | 122.53 | 3.4 | 22.5 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 100.00 | 105.02 | 105.66 | 0.6 | 5.7 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 100.00 | 107.90 | 109.56 | 1.5 | 9.6 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 100.00 | 118.67 | 121.69 | 2.5 | 21.7 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 100.00 | 113.31 | 114.23 | 0.8 | 14.2 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 100.00 | 101.99 | 102.29 | 0.3 | 2.3 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 100.00 | 109.99 | 110.78 | 0.7 | 10.8 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 100.00 | 98.25 | 98.23 | 0.0 | -1.8 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 100.00 | 101.00 | 101.08 | 0.1 | 1.1 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 100.00 | 105.79 | 105.79 | 0.0 | 5.8 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 100.00 | 109.93 | 111.53 | 1.5 | 11.5 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 100.00 | 103.85 | 106.47 | 2.5 | 6.5 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100.0** | **100.00** | **114.08** | **116.80** | **2.4** | **16.8** |
| **Makundi mengine teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 100.00 | 117.56 | 121.32 | 3.2 | 21.3 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 100.00 | 128.61 | 133.06 | 3.5 | 33.1 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 100.00 | 109.96 | 111.45 | 1.4 | 11.4 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 100.00 | 107.15 | 108.20 | 1.0 | 8.2 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa wa mwaka unapima kiwango cha badiliko la bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, mfumuko wa bei wa Taifa kwa mwezi Septemba 2011 umeongezeka hadi asilimia 16.8 ikilinganishwa na asilimia 14.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2011. Kwa ujumla Fahirisi za bei zimeongezeka hadi 116.80 mwezi Septemba 2011 kutoka 100.00 mwezi Septemba 2010. Vyakula na vinywaji baridi vimeongezeka hadi asilimia 22.5 kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba 2011 kutoka asilimia 18.6 mwezi Agosti 2011.

### Mfumuko wa bei kwa bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula


Badiliko la Fahirisi ya bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limeongezeka hadi asilimia 21.3 kwa mwaka ulioishia Septemba 2011 ikilinganishwa na asilimia 17.4 kwa mwaka ulioishia Agosti 2011. Kasi ya ongezeko kwa bidhaa zisizo za vyakula imeongezeka hadi asilimia 11.4 kwa mwaka ulioishia Septemba 2011 kutoka asilimia 10.2 kwa mwaka ulioishia Agosti 2011.

### Mfumuko wa bei wa bidhaa na huduma zote isipokuwa bidhaa za vyakula na nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa majumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa watunga sera.

Mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwaka ulioishia Septemba 2011 umeongezeka hadi asilimia 8.2 kutoka asilimia 7.3 kwa mwaka ulioishia Agosti 2011. Mfumuko wa bei wa nishati umeongezeka hadi asilimia 33.1 kwa mwaka unaoishia Septemba 2011 kutoka asilimia 30.1 mwezi Agosti 2011.

### Kielelezo 1: MWELEKEO WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA NA MFUMUKO WA BEI KUTOKA SEPTEMBA, 2010 HADI SEPTEMBA, 2011. (SEPTEMBA 2010 = 100)




Kielelezo 1 hapo juu kinaonesha kumekuwa na mwenendo imara wa fahirisi za bei za taifa kutoka mwezi Septemba 2010 hadi Novemba 2010. Fahirisi zinaonesha kuongezeka sana kwenye miezi ya Desemba 2010 hadi Septemba 2011. Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei ulipungua hadi asilimia 4.2 mwezi Oktoba 2010 na umeanza kuongezeka hadi kufikia asilimia 16.8 mwezi Septemba 2011.

### MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 2.4

Mfumuko wa bei wa mwezi Septemba 2011 umeongezeka kwa asilimia 2.4, Fahirisi za bei zimeongezeka hadi 116.80 mwezi Septemba 2011 kutoka 114.08 mwezi Agosti 2011. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kumechangiwa hasa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa bei ni pamoja na mikate kwa asilimia 1.5, vitafunwa kwa asilimia 1.8, mahindi kwa asilimia 5.1, unga wa mihogo kwa asilimia 2.2, nyama kwa asilimia 5.1, samaki kwa asilimia 6.0, maziwa kwa asilimia 2.9, mafuta ya kupikia kwa asilimia 2.7, matunda kwa asilimia 4.6, sukari kwa asilimia 16.4, juisi za matunda kwa


asilimia 4.0. Bidhaa zisizo vyakula ni pamoja na mavazi kwa asilimia 4.9, mavazi ya watoto kwa asilimia 1.6, gesi kwa asilimia 11.0, mkaa kwa asilimia 8.3, makochi ya sofa kwa asilimia 4.0 na gharama ya kusaga mahindi kwa asilimia 3.4.

## Thamani ya Shilingi 100 mwezi Septemba 2010 ikilinganishwa na mwezi Septemba 2011

Thamani ya shilingi 100 imepungua kutoka mwezi Septemba 2010 hadi kufikia shilingi 82 na senti 09 mwezi Septemba 2011.

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo 2: Mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya Fahirisi za bei




Kielelezo namba 2 hapo juu kinaonesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei; fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi cha miezi saba iliyopita zikilinganisha na fahirisi zingine isipokuwa kwa mwezi Aprili mpaka Septemba 2011, kwa upande mwingine kundi la nishati na mafuta limekuwa na fahirisi za juu kuliko makundi mengine katika kipindi hicho. Kwa kipindi cha miezi 12, kundi la nishati na mafuta limeonesha kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano:** **Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**